Uzimaji Moto: Mchango Mkubwa Katika Ajira ya Vijana Nchini Afrika Kusini

Wazima Moto wakiwa kwenye mstari wa kuuzima moto hivi majuzi ulioanza katika eneo la Muizenberg. Picha ni kwa Hisani ya: IPS-WoF1

CAPE TOWN, Afrika Kusini, Januari, 20 2016 (IPS) - Nolukhanyo Babalaza alikamilisha mwaka wake wa mwisho wa masomo ya shule ya upili na kupokea stashahada yake mwak6a wa 2000, lakini stashahada hii haikuwa kibali cha maisha mema. Babalaza alikufa moyo kuona kwamba kuna wale waliokuwa wamefanikiwa huku yeye alikuwa akiumia ili kuweza kukimu mahitaji msingi kama vile chakula cha kila siku.

“Hali hii humpa mtu mawazo mabaya. Mwishowe, mtu hufanya mambo ambayo yeye hujuta baadaye” Babalaza alisema.

Hatimaye, baada ya miaka mitatu mlango wa Babalaza ukafunguka. Babalaza alipata kuwa mmoja wa watu wanaoshughulikia uzimaji moto. Babalaza alijiunga na Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (South Africa’s Department of Environmental Affair’s Working on Fire Programme (WoF).

Moto umekuwa tatizo lililokithiri nchini Afrika Kusini, moto huu huharibu maisha, mali na mazingira bila kuchagua.

Iwe wakati wa kipindi cha miezi ya jua kali katika eneo la Western Cape, au katika miezi ya Kipupwe katika sehemu nyingine za nchi, moto ulioenea huanzishwa na ngurumo za radi au, katika maeneo ya milima moto huanzishwa na mawe yanayoanguka au kwa ajali kama tokeo la watu wasiokuwa makini. Mamilioni ya mali hupotezwa kila mwaka. Maisha ya watu na wanyama na mazingira huharibiwa.

Hata hivyo, mambo mazuri yameibuka kutokana na tatizo hili la kila mwaka.

Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (WoF) iliyoanzishwa mwaka wa 2003 imekuwa kama mbinu ya kukumbana sio tu na moto bali pia kukumbana na masuala magumu ya ukosefu wa ajira na umaskini.

Vijana wengi wameondoelewa kutoka katika hali za ukosefu wa ajira na umaskini.

“Vijana hawa hupewa mafunzo ili kuwasaidia katika kukumbana na moto isioyotarajiwa katika mbuga na moto msituni Afrika Kusini kote na mara nyingi vijana hawa hutumia ujuzi wao kama ufunguo wa kujiunga na kazi za kirasmi,”anaeleza Linton Rensburg ambaye ni Msimamizi wa WoF wa Mawasiliano ya Kitaifa.

Vijana hawa hupewa mafunzo ya udereva, ukataji vichaka, uzimaji moto, usimamizi wa usalama wa helkopta na mafunzo katika elimu ya mazingira. Mafunzo katika nyanja hizi hayaleti pesa nyingi lakini yanawapa vijana mbinu za kushughulikia maisha yao ya baadaye.

Kulingana na takwimu za Uchumi wa Kibiashara, asilimia ya watu waliokosa ajira Nchini Afrika Kusini imeongezeka hadi asilimia 25.5 katika miezi mitatu ya mwisho ya mwaka wa 2015 kutoka asilimia 25 katika kipindi cha awali cha miezi mitatu. Kiwango cha ukosefu wa ajira kilipanda kwa asilimia 3.6 huku kiwango cha ajira kikipanda kwa asilimia 1.1 na watu wengi zaidi waliajiriwa. Kutoka mwaka wa 2001 hadi mwaka wa 2015, kiwango wastani cha ukosefu wa ajira nchini Afrika Kusini ni asilimia 25.27, kiwango cha juu zaidi cha ukosefu wa ajira kilichoshuhudiwa ni cha asilimia 31.20 katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka wa 2003 huku kiwango cha chini cha ukosefu wa ajira kilichowahi kushuhudiwa ni cha asilimia 21.50 katika miezi mitatu ya mwisho ya mwaka wa 2008. Deta ya viwango vya ukosefu wa ajira nchini Afrika Kusini inaripotiwa na Shirika la Takwimu la Afrika Kusini.

Wafanyakazi wa Kuzima Moto

Babalaza amekua kadri programu hii imeendelea kukua. Alianza kama anayezima moto akapanda cheo hadi msimamizi wa kikundi na kisha akapanda cheo zaidi na kuwa msimamizi msaidizi. Leo hii yeye ni afisa msimamizi wa fedha katika programu hii mjini Western Cape.

Babalaza anakiri kwamba programu hii imeboresha maisha yake kwa kiwango kikubwa mno.

“Mambo ni bora zaidi. Angalau ninaweza kukidhi mahitaji ya familia yangu na pia kulipa gharama zangu za kila mwezi,” Babalaza alieleza.

Rensburg alielezea IPS kwamba hadithi ya Babalaza ni moja miongoni mwa vijana wengi wanaohusishwa katika programu hii ya uzimaji moto.

“Maelfu ya vijana wamepata nafasi za kazi zenye manufaa katika programu hii na baada ya kupitia mafunzo na vipengele vya ukuzaji ujuzi vya Programu za Moto (WoF), vijana hawa wameweza kuendelea kutoka wazima moto wanaopata ujira hadi wafanyakazi wa Programu za Moto (WoF) wanaolipwa mshahara kila mwezi,” Rensburg alisema.

Zingatia hadithi ya Justine Lekalakala kwa mfano. Lekalakala ambaye alianza kama mtu anayezima moto katika Kitengo cha Dinokeng mjini Hammanskraal Kaskazini mwa Pretoria, sasa anafanya kazi katika Jeshi la Kitaifa la Afrika Kusini.

“Niliweza kutumia malipo ambayo nilipata nilipokuwa ninafanya kazi katika Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (WoF), kutuma maombi ya kazi nyinginezo na kujielimisha kwa kusoma kozi za kompyuta. Ilikuwa rahisi kwangu kuingia katika jeshi kwa kuwa nilikuwa mwenye nidhamu ya hali ya juu na mwenye afya njema kimwili, vitu hivi viwili nilivipata kutokana na mimi kufanya kazi katika Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (WoF),” Lekalakala alieleza.

Christalene De Kella hakuwa na uhakika wa nini alichotaka katika maisha yake baada ya kukamilisha masomo yake ya shule ya upili katika mwaka wa 2004. Alichukua fursa ya kuwa mzima moto katika mji wake wa nyumbani wa Uniondale. Mama huyu mlezi wa pekee wa mtoto wake wa kike wa miaka 7, sasa ameanzisha mwelekeo wake wa maendeleo na kazi anayotaka kufanya katika siku zijazo.

Akianzia kiwango cha Mzima moto, Christalene De Kella amesoma kozi za udhibiti wa moto na hata kushiriki katika kufungua, kambi mpya. Katika mwaka wa 2005, Christalene De Kella alipandishwa cheo na kuwa msimamizi wa vifaa wa Programu za Moto (WoF).

Mnamo mwaka wa 2009, Kella alipata kazi ya kuwa mwanahabari na afisa wa kijamii katika eneo la Southern Cape na katika mwaka wa 2013, Kella alipewa fursa ya kuwa mwanahabari wa kitengo cha video cha Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (WoF).

“Kufanya kazi ya kuzima moto kumekuwa na athari nzuri katika maisha yangu,” Kella alisema huku akiongeza kwamba yeye husafiri nchini kote ili kuhoji na kurekodi hadithi zitakazotumika katika habari za televisheni ya Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (WoF) kwenye YouTube.

Ukuaji huu hauwezi kukosa kufafanuliwa bila kuzingatia wazima moto wawili wa awali ambao walianza mafunzo yao ya miaka miwili ya kuwa marubani katika Shule ya Marubani mjini Mbombela, Mpumalanga.

Themba Maebela, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Mpumalanga na Siyabonga Varasha mwenye umri wa miaka 26, kutoka eneo la Cape Mashariki wameajiriwa kama wasaidizi wa kibinafsi.

“Ilikuwa kana kwamba nilikuwa naota familia yangu haikuniamini wakati nilipowaambia kwamba nitapata mafunzo ya kuwa rubani, Maebela ambaye alijiunga na kitengo cha kuzima moto mnamo 2010 alieleza.

Vijana wa Afrika Kusini ambao hawana stashahada inayohitajika lazima watoe matokeo mema zaidi katika kazi zao na waajiri wao watatambua vipawa na ujuzi wao, Maebela alihimiza vijana.

Naome Nkoana anapoendelea kukagua mitaa kama askari wa mji wa Pretoria anakumbuka namna ushiriki wake katika Programu za Moto (WoF) ambapo alipata mafunzo ya kina zaidi ya udereva mjini Nelspruit, ulivyomsaidia sio tu kupita mitihani ya kuwa polisi bali pia kuboresha ujuzi wake wa udereva na kumrahishia kuweza kujiunga na idara ya polisi kama polisi wa mji mkuu kama vile Pretoria.

Rensburg anasema kwamba tangu Programu ya Kushughulikia Moto ilipoanzishwa, programu hii imebadilisha maisha ya washiriki 5000 moja kwa moja na kunufaisha wategemezi wengine 25,000 wa washiriki hawa kwa njia zisizo za moja kwa moja.

Utafiti wa Mwaka wa 2012 wa Athari za Kijamii za Programu za Moto kwa washiriki ulionyesha kwamba mafunzo yanayowasilishwa na Idara ya Afrika Kusini ya Masuala ya Kimazingira Inayoshughulikia Programu za Moto (WoF) yaliyanufaisha maarifa ya washiriki na kukuza uwezo wa kufahamu umuhimu wa kila mmoja wa washiriki katika ujenzi wa nchini miongoni mwa washiriki.

Utafiti ulihitimisha kwamba “Kupitia Programu za Moto (WoF),vijana hawa waliweza kufahamu upungufu na uwezo wao vyema zaidi.”

(Mwisho)